

Matumizi ya Kiswahili katika Bidhaa za Watoto Nchi Tanzania: Yaliyomo na Yasiyokuwamo

Shadidu Abdallah
Chuo Kikuu cha St. John's, Tanzania

Ikisiri

Makala haya ni sehemu ya utafiti uliofanyika katika Jiji la Dodoma. Utafiti uliongozwa na malengo makuu matatu. Mosi, kubainisha bidhaa za watoto na kutoa tathmini ya jumla kuhusu hali ilivyo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Pili, kuonesha lugha zinazotumika katika bidhaa za watoto. Tatu, kujadili umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika bidhaa za watoto. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji data ni udurusu wa kimaktaba na ushuhudiaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Kiswahili hakijatumika kwa kiasi kikubwa katika bidhaa za watoto. Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kichina na Kituruki zimeonekana kutawala katika bidhaa za watoto nchi Tanzania. Hali hii inakidunisha Kiswahili na kuzipa hadhi kubwa lugha za nje. Aidha, kwa upande wa walaji/watumiaji wa bidhaa, matumizi ya lugha za kigeni yanaweza kuwa hatari kiusalama kwa kuwa, wanatumia bidhaa ambazo hawajui matumizi yake kiusahihi.

Maneno Muhimu: Kiswahili, Bidhaa, Watoto, Tanzania

Utangulizi

Watoto ni sehemu muhimu ya jamii yoyote duniani. Kwa mujibu wa takwimu za kidunia, zaidi ya nusu ya watu wote duniani ni watoto. Kutokana na umuhimu wa kundi hili zipo sheria na kanuni mbalimbali zilizotungwa ili kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa na kupata mahitaji yao ya msingi bila kubaguliwa. Katika maisha, yapo mahitaji muhimu kwa ustawi wa watoto. Miongoni mwa mahitaji ya msingi ya watoto ni pamoja na malazi, chakula na mavazi (*Tanzania Law Society*, 2016 na Shima 2012). Aidha, kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989, ni jukumu la serikali na jamii kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu, mapenzi, huduma ya afya na ulinzi popote walipo. Kufanikisha haya yote, lugha ya mawasiliano mapana ni kitu cha muhimu sana. Jamii mbalimbali duniani zinatumia lugha zao kama nyenzo ya mawasiliano. Kwa upande wa Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha rasmi ya mawasiliano mapana (Qorro, 2003 na Lupogo, 2014). Hii ni kusema kuwa, Kiswahili ni lugha ya taifa, hivyo,

hutumika kama lugha rasmi serikalini, bungeni, katika mahakama za awali na katika vyombo vya habari. Pia, Kiswahili ndiyo lugha inayotumika sana katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi miongoni mwa wanajamii (Rubagumya, 2003 na Vuzo, 2005).

Pamoja na umuhimu huu wa lugha ya Kiswahili, bado kumekuwa na ulegevu katika kukitumia kwenye baadhi ya maeneo. Hii ni kusema kuwa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zimeendelea kupewa nafasi kubwa ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili (Rubagumya, 1991). Miongoni mwa maeneo ambayo lugha ya Kiswahili imekuwa ikiwekwa kando ni katika bidhaa mbalimbali za watoto. Pamoja na kuwa serikali na idara zake zimekuwa zikisisitiza matumizi ya Kiswahili (tafsiri) katika bidhaa mbalimbali, bado juhudi hizi hazijazaa matunda. Bidhaa nyingi za watoto zinazotumika nchini Tanzania zimekuwa zikitambuliwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kichina, Kituruki n.k. Matumizi ya lugha hizi yanaviza na kudunisha maendeleo ya Kiswahili na kuhatarisha maisha ya watumiaji (Waswahili). Hivyo basi, makala haya yanatalii matumizi ya Kiswahili katika kutaja bidhaa za watoto, kwa kubainisha hali ilivyo na kuonyesha umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika bidhaa hizo.

Hali Ilivyo

Katika maduka mbalimbali yenye kuuza bidhaa za watoto nchini Tanzania, bidhaa za watoto zinaweza kugawanywa katika migao mwili. Katika mgao wa kwanza ni kuzigawa bidhaa kwa namna ya matumizi (matumizi ya ndani na matumizi ya nje). Hivyo basi, tunapata kuwa kuna bidhaa za chakula na bidhaa nyinginezo. Bidhaa za chakula ni zile ambazo hutumika kwa matumizi ya chakula na lishe kama vile maziwa, biskuti, pipi, nafaka, maji, soda n.k. Pia, bidhaa za chakula hujumuisha bidhaa zinazotumika kwa ajili ya matibabu hasa madawa ambayo hutumika kutibu maradhi mbalimbali yanayowasumbua watoto. Aina ya pili ni zile bidhaa za watoto zisizoliwa. Katika kundi hili tunapata bidhaa mbalimbali muhimu za watoto kwa matumizi mengine yasiyo ya chakula kama vile nguo, viatu, midoli, mabegi, kandambili, magari, nepi, vitaulo vya watoto (*baby wipes*), nk.

Katika mgao wa pili, tunazigawa bidhaa za watoto kwa kuzitazama bidhaa za watoto kwa mahali zilipotengenezwa. Kwa kutumia kigezo hiki, katika maduka yetu, bidhaa za watoto zinazouzwa zimegawanyika katika namna mbili. Aina ya kwanza ni zile bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania. Zipo bidhaa za kutosha ambazo hutengenezwa nchini Tanzania na ni maalum kwa ajili ya watoto. Bidhaa hizi zina ubora sawa na bidhaa zingine zilizopo madukani. Aidha, baadhi ya bidhaa hizi ni bora kuliko hata bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Aina ya pili ni bidhaa ambazo hutoka nje ya nchi. Baadhi ya nchi ambazo bidhaa zao za watoto zimesheheni madunikani ni pamoja na China, Uturuki, Kenya, Afrika Kusini, India, Uingereza na Misri.

Kwa jumla, kwa kuangalia katika migawanyo yote miwili ya bidhaa za watoto, kuna matumizi makubwa ya lugha mbalimbali. Matumizi hayo ya lugha yamelenga kuhakikisha kuwa mtumiaji wa bidhaa husika wanapewa taarifa zote muhimu kuhusu bidhaa husika. Maelezo katika bidhaa hujiielekeza katika kufahamisha kuhusu matumizi sahihi ya bidhaa husika, komponenti mbalimbali zilizopo katika bidhaa husika, tahadhari kuhusu matumizi ya bidhaa, taarifa muhimu kuhusu kampuni inayotengeneza bidhaa, muda wa matumizi wa bidhaa husika n.k. Kwa hakika, hizi ni taarifa muhimu kwa watumiaji wa bidhaa yoyote ile. Ni haki ya mtumiaji kujua kuhusu anachokitumia. Kukosa taarifa kuhusu bidhaa husika ni hatari na kunaweza kuleta madhara makubwa kwa mtumiaji. Pamoja na ukweli huu, hali ilivyo katika bidhaa zilizopo madukani haziakisi ukweli huu. Hii ni kusema kuwa bidhaa nyingi zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kituruki na Kiarabu. Kwa kuzingatia kuwa zaidi ya asilimia tisini ya Watanzania wanatumia lugha ya Kiswahili katika maisha yao ya kila siku, kukithiri kwa matumizi ya Kiingereza katika bidhaa za watoto nchini Tanzania ni jambo la kushtua, kushangaza na linalohitaji tafakuri kubwa.

Inafahamika kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa. Kwa hali hii, Kiswahili ni lugha rasmi ya mawasiliano mapana nchini Tanzania. Hivyo basi, ingelifaa taarifa muhimu zilizo katika bidhaa za watoto ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili. Jambo la kushangaza ni kuwa, hata zile bidhaa zinazozalishwa nchini Tanzania bado zinaangukia katika mkumbo huu wa kutumia lugha za wageni. Kwa mfano, Diamond Karanga¹ ni bidhaa maarufu miongoni mwa watoto nchini Tanzania. Pamoja na kuwa bidhaa hii inaweza kutumiwa na watu wa rika zote, bado watoto hasa wale wa shule za msingi ndio watumiaji wakubwa wa bidhaa hii. Cha kushangaza ni kuwa katika bidhaa hii, ukiachilia mbali neno karanga, lugha ya Kiswahili haijatumika kabisa. Bidhaa hii inauzwa Tanzania, wanunuzi wake ni Waswahili ambao wangesikia fahari kuelewa kilichoandikwa katika bidhaa inayotengenezwa na Mswahili mwenzao.

¹ Diamond Karanga ni bidhaa inayomilikiwa na msanii maarufu wa Tanzania akifahamika kwa jina la Diamond Platnumz. Msanii huyu amejipatia umaarufu kupitia muziki wake anaomba kwa lugha ya Kiswahili. Wateja wakubwa wa Diamond Karanga ni watoto na vijana.



Kilelelezo: Picha ikionesha maelezo muhimu katika bidhaa ya Diamond Karanga

Bidhaa hii inatengenezwa Tanzania lakini maelezo yote yametolewa kwa lugha ya Kiingereza. Pamoja na changamoto hii, zipo bidhaa chache zinazotoka nje ambazo zimetafsiri baadhi ya maelezo yao kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Bidhaa hizi ni pamoja na maziwa na nafaka kwa ajili ya watoto wachanga. Pamoja na kupongeza juhudi hizi nzuri, bado zipo changamoto kadhaa katika tafsiri hizi. Kwa mfano, zipo bidhaa hasa za maziwa ya unga na nafaka (*cereal*) ambazo zimetumia tafsiri tenge. Pia, tafsiri imetolewa kwa baadhi ya maelezo na kuacha mengine hata kama ni ya muhimu. Kwa upande wa madawa yanayotoka nje, lugha inayotumika kwa kiasi kikubwa ni Kiingereza. Tofauti na ilivyo katika bidhaa za maziwa na nafaka, kwa upande wa madawa, sheria haiwalazimishi watengenezaji kutumia lugha ya Kiswahili. Hoja kuu hapa ni kuwa bidhaa za madawa hupaswa kutolewa na mtaalamu yaani mfamasia ambaye bila shaka atakuwa anaifahamu vyema lugha ya Kiingereza. Pamoja na ukweli huu, bado kuna umuhimu mkubwa wa kutumia lugha ya Kiswahili katika madawa (hasa ya watoto) yanayotumika nchini Tanzania. Hii ni kwa kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka vizuri miongoni mwa wafamasia na wagonjwa. Aidha, katika maendeleo ya vijijini na hata katika baadhi ya miji midogo, kuna uwezekano wa bidhaa hizi kuuzwa na watu ambao hawana sifa za kutosha kuwa wafamasia. Hivyo basi, kama lugha ya Kiswahili itatumika katika bidhaa, itasaidia jamii kuelewa matumizi sahihi ya madawa husika.



Kielelezo: Picha inayoonesha matumizi ya tafsiri tenge katika bidhaa za watoto

Watengenezaji wametumia tafsiri ya neno kwa neno. Neno **nepi** lenyewe limeachwa na wametumia istilahi pumkini ambayo sio neno rasmi.

Kuhusu Lugha Zinazotumika katika Bidhaa za Watoto

Katika bidhaa za watoto zinazotumika katika jiji la Dodoma, ni wazi kuwa lugha ya Kiingereza imetumika kuliko lugha nyingine ikifuatiwa na Kifaransa, Kiarabu, Kichina na Kituruki. Lugha ya Kiingereza imetumika sana kutokana na sababu kuu tatu. Mosi, kama tulivyosema hapo nyuma ni kuwa bidhaa hizi nyingi zimetengenezwa katika nchi ambazo lugha yao kuu ya mawasiliano ni Kiingereza. Nchi hizo ni pamoja na Uingereza, Afrika Kusini na Kenya. Pili, katika baadhi ya bidhaa, Kiingereza kimetumika kama lugha muhimu ya tafsiri. Katika eneo hili tunapata bidhaa zinazotengenezwa na Uturuki na China. Kwa mfano, bidhaa kama *Preto Baby* na *Molfix* zimetumia lugha ya Kituruki kama lugha ya kwanza na Kiingereza kimetumika kama lugha ya tafsiri. Tatu, zipo bidhaa zilizotumia lugha ya Kiingereza kwa namna ya mazoea tu. Katika kundi hili tunapata bidhaa zinazotengenezwa hapa Tanzania na kuuzwa hapahapa kwa ajili ya Watanzania, lakini zimetumia lugha ya Kiingereza pekee. Kwa mfano, bidhaa kama *Diamond Karanga* imetumia lugha ya Kiingereza kwa namna ya mazoea tu.

Kwa kuzingatia kuwa bidhaa inalenga watumiaji wengi wa ndani ambao ni Waswahili, ilikuwa ni muhimu kutumia lugha yao ya Kiswahili. Pia, katika kundi hili tunapata bidhaa nyingi kutoka kampuni ya kama vile Azam Soda, Azam Embe, Azam Ice Cream, Azam Milk n.k. Kwa kuzitazama bidhaa hizi ni wazi kuwa wateja wake wakubwa ni watoto. Pamoja na kuwa bidhaa za Azam zinazotumika ndani na nje ya Tanzania, ukweli unabaki kuwa wateja wengi wa bidhaa hizi ni Watanzania ambao wangejisikia fahari kuona lugha yao inatumika katika bidhaa zinazotengenezwa na Waswahili wenzao. Aidha, matumizi ya lugha ya Kiswahili

katika bidhaa zinazotoka nje ya nchi kungeongeza juhudi muhimu ya kukitangaza Kiswahili huko nje. Kwa hali hii, ni wazi kuwa zipo bidhaa nyingi zinazotengenezwa na kuuzwa hapahapa nchini Tanzania lakini zimetumia kimazoea lugha ya Kiingereza. Tunasema zimetumia lugha ya Kiingereza kimazoea ili zifanane na bidhaa nyingine zilizopo madukani. Ni wazi kuwa wamiliki wa bidhaa hizi wamesahau kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha muhimu kwa watumiaji wengi wa bidhaa zao. Kwa kuzingatia kuwa Kiswahili ni lugha inayofahamika na wengi nchini Tanzania, kitendo cha kuithamini lugha ya Kiingereza na kukisahau Kiswahili katika maandishi ya bidhaa za Kitanzania kunavunja daraja muhimu la mawasiliano baina ya bidhaa zao na watumiaji (Rubagumya, 1990 na Qorro & Zaline, 1997). Pamoja na matumizi makubwa ya lugha ya Kiingereza katika bidhaa za watoto nchini Tanzania, bado kuna matumizi ya lugha nyingine za kigeni. Miongoni mwa lugha zinazotumika sana katika bidhaa hizo ni pamoja na Kichina, Kifaransa Kiarabu na Kituruki. Pamoja na kuwa hazijashamiri kama Kiingereza, zimepewa nafasi kubwa mno katika bidhaa za watoto zilizopo katika maduka yaliyopo katika jiji la Dodoma. Kukithiri kwa matumizi ya lugha hizi katika bidhaa za watoto kunaweza kuibua changamoto nyingi. Kwa mfano, ukiachilia mbali lugha ya Kiarabu, lugha ya Kituruki, Kifaransa na Kichina zina watumiaji wachache sana nchini Tanzania. Hivyo basi, kukithiri kwa matumizi yake katika bidhaa za watoto ni kuwanyima watumiaji fursa ya wazi kabisa ya kuelewe kile kilichoandikwa. Pamoja na ukweli huu, ni jambo la kushangaza kuona bidhaa za watoto kama vile *Predo Baby*, *Sleepy* na *Molfix* zimetumia maelezo mengi ya Kituruki bila kutoa hata tafsiri ya Kingereza achilia mbali tafsiri ya Kiswahili. Ni wazi kuwa asili ya bidhaa hizi imechangia matumizi ya lugha ya Kituruki. Pamoja na utetezi huu, tunaona ipo haja kwa wadau na serikali kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inapewa nafasi yake katika bidhaa hizi.

Kushamiri kwa lugha za kigeni katika bidhaa za watoto nchini Tanzania kunaonyesha wazi kuwa kuna udhaifu mkubwa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Swali la kujiuliza ni, kwa nini Kiswahili hakipewi nafasi yake katika bidhaa za watoto? Bila shaka zipo sababu kadhaa zilizotufikisha hapo. Kama mtu atajaribu kuzama kwa kina, bila shaka atabaini kuwa zipo sababu tatu ambazo zitajitokeza mara kwa mara. Mosi, hali ya kuthamini lugha za watu na kutokijali Kiswahili. Hali hii inaonekana vizuri katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye bidhaa za Kitanzania. Iltarajiwa kuwa, bidhaa zote zinazotengenezwa hapa Tanzania zingekuwa mfano kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kuwa watumiaji wake wengi wanajua lugha hiyo. Ukipita katika maduka ya kawaida kabisa nchini Tanzania utakuta bidhaa zinazotengenezwa na wajasiriamali wadogowadogo kama vile karanga, bisi, ubuyu, visheti, maandazi, vitumbua, ndizi za kukaanga, keki n.k. Bidhaa hizi zimewekwa katika vifungashio ili kuviongeza thamani sambamba na maelezo machache kuhusu taarifa za mtengenezaji, tarehe

ya kutengenezwa na kuharibika. Pamoja na kuwa bidhaa hizi huwalenga watumiaji Waswahili tena katika miji husika, bado watengenezaji wake wengi wameng'angania kutumia lugha ya Kiingereza. Kwa hakika, matumizi ya Kiingereza katika muktadha wa bidhaa zetu wenyewe ni jambo la kimazoea na kikasumba. Tumeamua kutumia lugha ya Kiingereza ili bidhaa zetu zifanane na zile za nje.

Pili, kukithiri kwa lugha ya Kiingereza kunasukumwa na hali ya kuwepo kwa bidhaa nyingi za watoto zinazotoka nje. Bidhaa hizi zimekuwa zikiandikwa kwa lugha za nchi hizo (Kiingereza, Kituruki, Kifaransa, Kiarabu na Kichina).

Kama tulivyosema huko nyuma, sababu hii ni ya kweli isipokuwa kuna umuhimu wa kuiondoshwa kwa kutumia mikakati maalum hasa sheria mbalimbali. Kwa mfano, nchini Tanzania, huko nyuma kumekuwa na sheria inayoyalazimu makampuni yenye kutengeneza maziwa na vyakula vya watoto wachanga kufanya tafsiri katika bidhaa zao. Kupitia sharia hii makampuni haya yamelazimika kuweka tafsiri katika bidhaa zao kwa lengo la kumlinda mlaji/mtumiaji. Kupitia kwa sharia hii, maziwa yote na vyakula vya watoto wachanga ambavyo havina tafsiri ya Kiswahili hunyimwa usajili. Pamoja na kuwa sharia hii haijaondoa kabisa maziwa na vyakula vya watoto wachanga vilivyoandikwa kwa lugha za kigeni, ni wazi kuwa kuna hatua muhimu iliyopigwa kupitia sharia hii. Hivyo basi, huu ni wakati muafaka wa kuhakikisha bidhaa zote za watoto zinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuhakikisha kuwa watumiaji wa bidhaa wanaelewa kila kinachoandikwa.

Tatu, ni kukosekana kwa mwamko wa kupenda kusoma taarifa muhimu za bidhaa miongoni mwa wanunuzi. Kumekuwa na kampeni nyingi zinazofanya, kupitia vyombo vya habari, mashule na mikutano ya hadhara, uhamasishaji wa wananchi wa Tanzania kutumia bidhaa halisi na kupiga vita bidhaa bandia. Kampeni hii imekuwa ikiongozwa na vyombo vya kitaifa vyenye dhamana kama vile Jeshi la Polisi, mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shrika la Ubora wa Viwango Tanzania (TBS). Miongoni mwa ajenda kubwa ya vyombo hivi ni kuhamasisha wananchi kusoma taarifa muhimu zilizomo katika bidhaa husika zikiwemo bidhaa za watoto. Aidha, wanaamini kuwa kutokana na wananchi kutopenda kusoma taarifa za bidhaa, imekuwa rahisi kwa wauzaji wasio waaminifu kuwauzia bidhaa bandia. Kutokana na hali hii, wanaamini kuwa hata lugha ya Kiswahili ikitumika katika bidhaa itakuwa ni kazi bure kwani hakuna wasomaji wa taarifa hizo.

Pamoja na maelezo hayo, ukweli unabaki palepale kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili ni jambo la muhimu na halipaswi kupuuzwa na kupaushwa kwa hoja zozote. Aidha, matumizi ya lugha ya Kiswahili ni kiungo muhimu katika vita dhidi ya bidhaa bandia kwa kuzingatia kuwa upo mkakati wa kiserikali kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Jeshi la Polisi na wadau wengine unaolenga

kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa halisi na kuepuka matumizi ya bidhaa feki/hafifu. Mpango huu unahimiza watumiaji kusoma maelekezo muhimu yaliyomo katika bidhaa ili kubaini kama bidhaa ni halisi au la. Ni wazi kuwa, matumizi ya lugha za kigeni kunafifisha juhudi hizi.

Umuhimu wa Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Bidhaa za Watoto

Upo umuhimu mkubwa sana wa kutumia lugha ya Kiswahili katika bidhaa zote za watoto ambazo zinazuwama madukani. Katika mjadala wetu tutataja sababu kuu tano zinazotusukuma kusema kuwa lugha hii ni muhimu zaidi kuliko hizo lugha nyingine. Mosi, ni suala la usalama wa walaji/watumiaji wa bidhaa. Ni wazi kuwa bidhaa nyingi za watoto zina maelekezo muhimu ambayo hupaswa kufuatwa kabla, wakati na baada ya kuzitumia. Kwenda kinyume na maelekezo huweza kusababisha madhara kwa watumiaji. Kwa mfano, baadhi ya maelezo yaliyopo katika nepi za watoto kama vile *Predo* na *Sleepy* yanataja muda maalum ambao mtoto anaweza kuzitumia bila kubadilishwa. Aidha, zinataja muda ambao mzazi anapaswa kuhakikisha kuwa mtoto amebadili nepi hizo. Pia, wanaelezea madhara ambayo mtoto anaweza kuyapata kama nepi hiyo haitabadilishwa. Hata hivyo, kwa kuwa lugha iliyotumika ni lugha za kigeni hasa Kituruki ambacho hakina wazungumzaji wengi nchini Tanzania, kuna uwezekano kwamba maelezo haya hayaeleweki na hivyo kusababisha watoto kupata madhara.



Kielelezo: Picha inayoonesha bidhaa kutoka nje ikiwa na maelezo ya lugha ya Kiingereza

Maelezo haya ni muhimu kwa mtumiaji hasa kwa mzazi/mlezi. Kutokana na lugha iliyotumika kuwa ni ya kigeni, kuna uwezekano mkubwa kwamba tahadhari zinazotolewa na watengenezaji zikapuuzwa na watumiaji, hali inayoweza

kusababisha madhara kwa watumiaji wa bidhaa hizo. Pia kuna maziwa ya watoto wachanga kama vile *SMA* ambayo hayana maelezo ya Kiswahili. Kwa kuzingatia kuwa maziwa haya yana viwango na namna maalum ya kutumika, kuna hatari kubwa kwa watumiaji kushindwa kuzingatia na kuleta madhara kwa watoto. Kwa mfano, katika maziwa ya SMA kuna sehemu iliyoandikwa “*Do not change proportions without medical advice*” yaani usibadili viwango (vya matumizi) bila ushauri wa daktari. Maelezo haya ni machache lakini ni muhimu sana kwa mtumiaji wa maziwa husika. Maelezo yanatoa tahadhari muhimu kwa mzazi/mlezi au mtu mwingine yeyote kuwa anapaswa kuzingatia viwango vilivyoidhinishwa kwa usalama na afya ya mtoto wake.

Kwa upande mwingine zipo bidhaa za maziwa na nafaka ambazo zimetafsiriwa kwa Kiswahili. Pamoja na kuwa tafsiri zao zina changamoto za hapa na pale, bado zinakidhi haja na zinawapa mwanga mkubwa watumiaji wa bidhaa hizo. Kwa mfano, katika maziwa ya *Infacare*, kuna maelezo muhimu kuhusu namna bora ya kuchanganya maziwa (uwiano wa maji na maziwa), maji yanayofaa kutumika, hali ya usafi wa vyombo, umri wa mtoto unaofaa kutumia bidhaa husika, muda wa kutengenezwa bidhaa na kuda wa mwisho kutumika. Ni wazi kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili yatawarahisishia wauzaji na watumiaji wa bidhaa kujua namna bora ya kutumia bidhaa husika.


Tatu, matumizi makubwa ya lugha za kigeni katika bidhaa zetu ni ishara ya kutokithamini Kiswahili na kutukuzia lugha za watu. Kiswahili kimekuwa na kinapaswa kuaminiwa katika maeneo yote nchini Tanzania. Kwa sasa Kiswahili ni lugha rasmi ya Umoja wa Afrika (AU), Lugha Rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia ni lugha rasmi nchini Tanzani, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Kongo. Kitendo cha kukinyima fursa ya kutumika katika bidhaa za watoto ni dalili kuwa tunaendeleza kasumba ya kutokiamini. Pia, tunatoa ishara mbaya kwa watoto wetu ya kuwa, lugha ya Kiswahili haiwezi kutumika katika mambo muhimu. Watoto wanakuwa katika hali ya kuona bidhaa zao zote muhimu zimeandikwa kwa lugha za watu. Kwa hali hii, itakuwa kazi kubwa kuwaaminisha kuwa Kiswahili ni lugha muhimu inayoweza kutumika katika sehemu muhimu. Ni jukumu la wadau wote (serikali, watengenezaji bidhaa, wafanyabiashara na wapenzi wote wa Kiswahili) kuondoa hali hii kwa maendeleo ya lugha yetu.

Nne, kuna umuhimu wa kutumia Kiswahili katika bidhaa za watoto kwa sababu ndiyo lugha muhimu na inayotumiwa sana na watu wengi. Hakuna ubishi kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo lugha inayoeleweka vizuri nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Mlama na Matheru (1977) na Qorro (2003) lugha ya kiswahili ni muhimu kwa matumizi rasmi na yasiyo rasmi. Aidha, Mwansoko (1996), Mshindo (2010) na Mpemba (2013), wanaona kuwa lugha ni chombo muhimu cha mawasiliano. Ni jambo la kustaajabisha kuwa, pamoja na kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayotumika na kueleweka vyema katika mazingira yote nchini Tanzania bado kimeminywa mbavu katika bidhaa za watoto. Aidha, ni jambo la kushangaza

kuona bidhaa nyingi za watoto zinatumiya lugha ambazo hazina wazungumzaji kabisa nchini Tanzania. Kwa mfano, katika madawa muhimu ya watoto kama vile paracetamol na dawa za kikohozi zinazotoka nje hakuna kabisa maneno ya Kiswahili. Ni kweli kabisa kuwa lugha ya Kiingereza ni lugha ya kimataifa na kwa kiasi fulani inafahamika miongoni mwa Watanzania. Pamoja na haya yote haiondoi ukweli kuwa lugha hii ni lugha ya kigeni na haifahamiki kwa Watanzania wote. Sambamba na Kiingereza kuna matumzi ya lugha ambazo zina wazungumzaji wachache sana nchini Tanzania kama vile Kituruki, Kifaransa na Kichina. Swali la msingi hapa ni je, matumizi ya lugha hizi katika bidhaa za watoto yanamnufaisha nani? Au yamewekwa kama mapambo ambayo hayana umuhimu wowote? La hasha! kama tulivyosema huko nyuma zipo taarifa muhimu sana zinazoandikwa katika bidhaa. Hivyo, kutumia lugha ambazo watumiaji karibu wote hawaelewi ni kuwanyima fursa kujua taarifa muhimu zilizoandikwa. Ni muhimu kwa wadau wote wanaohusika na bidhaa za watoto kutazama hili ili kuhakikisha kuwa lugha inayotumika inafahamika kwa watumiaji. Nje ya hapo ni kusema kuwa Kiswahili kitaendelea kutupwa kando, tutawanyima watu wetu taarifa muhimu na huenda wakapata madhara makubwa kwa kukosa taarifa.

Tano, ni muhimu kuhamasisha matumizi ya Kiswahili katika bidhaa za watoto kwa lengo la kukuza ajira kupitia lugha ya Kiswahili. Kitendo cha kuendelea kutumia lugha za watoto ni sawa na kuuza soko la wataalamu wetu wa tafsiri, ukalimani, wahariri na wabunifu wengine. Ni muhimu kujua kuwa zipo fursa nyingi kupitia lugha ya Kiswahili hasa katika uga wa tafsiri na ukalimani (Wanjala, 2002 na Mshindo, 2010). Bidhaa zilizo madukani ni nyingi sana na nyingi hazitumii hata neno moja la Kiswahili. Swali la kujiuliza ni je, kama kungekuwa na mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinatumiya lugha ya Kiswahili tungeweza kutengeneza ajira kiasi gani kwa wataalamu wetu wa tafsiri na ukalimani waliopo Tanzania na Afrika Mashariki kwa jumla? Ni dhahiri kuwa kazi nyingi zingepatikana na zingewafaa sana watu wetu. Upo uoga kuwa kama tutawalazimisha, watengenezaji wanaweza kutoroka na hivyo tukakosa bidhaa zilizo bora. Huu ni uoga usiofaa. Duniani kote makampuni yanatafuta masoko na kuwafikia wateja wengi zaidi. Katika kuwafikia huko, lugha imekuwa kiungo muhimu sana baina ya mteja na mtengenezaji wa bidhaa. Ni muhimu ifahamike kuwa idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili duniani imekuwa ikiongezeka kila kukicha. Idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili ni mtaji tosha wa kuwafanya watengenezaji wa bidhaa kuitumia Kiswahili. Pia, upo mfano mzuri unaoweza kujionesha kupitia sharia ya Tanzania kuhusu maziwa na vyakula vya watoto wachanga. Kupitia sharia hii, makampuni yamelazimishwa kutumia lugha ya Kiswahili ili kuhakikisha kuwa watumiaji wanapata uelewa wa kile kilichoandikwa katika bidhaa. Pamoja na upinzani ulioikumba sharia hii hapo mwanzoni, hivi sasa maziwa yaliyotafsiriwa yamekuwa na soko kubwa na yanaaminika zaidi kwa

watumiaji. Mfano huu unapaswa kuwa alama muhimu ya kuongeza mapambano ya kuhakikisha kuwa bidhaa zote za watoto zinatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.



Kielelezo: Picha ikionesha mafuta ya kujipaka kwa ajili ya watoto

Maelezo yote muhimu katika mafuta haya yametolewa kwa Kiingereza. Mafuta haya yanatengenezwa na kampuni ya Chemi & Cotex Industries Ltd ya Dar es Salaam.

Hitimisho

Kuna haja ya kuimarisha sheria ili bidhaa zote zinazoingizwa au kutengenezwa hapa nchini Tanzania ziwe na tafsiri. Ni muhimu kujua kuwa biashara za wakati huu zina ushindani mkubwa. Makampuni yamekuwa yakibuni mbinu mbalimbali za kuwafikia wateja na kuzitangaza bidhaa zao. Njia rahisi ya kuwafikiwa wateja ni kutumia lugha za wazawa. Tumeona hali hii kupitia kwa makampuni makubwa kama vile CocaCola, Pepsi, Emirates Airways, Turkish Airways, n.k. Pia, hivi karibuni mashirika makubwa ya utangazaji yamekuwa yakitumia lugha ya Kiswahili katika matangazo yao. Kwa mfano, kampuni ya *Super Sport* imekuwa miongoni mwa kampuni ya mwanzo dunia kutumia Kiswahili katika matangazo ya Kombe la Dunia na ligi kuu ya Uingereza kupitia televisheni zake. Hivyo, ni jukumu la wahusika kusimamia sheria hizi ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inapata nafasi yake inayostahili. Kuendelea kutumia lugha za watu katika bidhaa ni kukidumaza Kiswahili na kuwanyika haki wazawa kujua kilichoandikwa katika bidhaa za watoto wao.

Marejeleo

- Lupogo, I. (2014). Language of Instruction: A Challenge for Secondary Schools and Tertiary Institutions in Implementing VET in Tanzania. Katika *Journal of Educational Policy and Entrepreneurial Research (JEPER)*, Juzuu , Uk. 26-30.
- Mlama, P., & Matteru, M. (1977). *Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Elimu ya Juu. A Research Report Commissioned by BAKITA, Dar es Salaam, Tanzania.* Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Mpemba, T. (2013). “Hali ya Taaluma ya Ukalimani Tanzania: Jana, Leo na Kesho” katika *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Juz. 76, Uk. 111-139.
- Mshindo, H.B. (2010). *Kufasiri na Tafsiiri*, Zanzibar: Kiwanda cha Uchapaji Chuo Kikuu cha Chukwani.
- Mwansoko, H.J.M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiiri: Nadharia na Mbinu*, Dar es Salaam: TUKI.
- Qorro, M. (2003). Unlocking Language Forts: The Language of Instruction in Post Primary Education in Africa with Special Reference to Tanzania. Katika Brock-Utne, Birgit, Zubeida: *LOITASA Research in Progress*. Dar es Salaam: KAD Associates.
- Qorro, M., Zaline, M., & Roy- Campbell, S. (1997). *Language Crisis in Tanzania. The Myth of English Versus Education*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Rubagumya, C. (1990). *Language in Education in Africa*. Clevedon: Multilingual Methods Ltd.
- Rubagumya, C. (1991). Language promotion for educational purposes: The example of Tanzania. *International Review of Education*, 37(1), 67-87.
- Shima, G. (2012). “Nafasi ya Vielelezo katika Fasihi ya Watoto”. Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Tanganyika Law Society (TLS). (2016). *Mtoto na Haki Zake: Sheria katika Lugha Rahisi*. Dar es Salaam: TLS.
- Vuzo, M. (2005). Using English as a Medium of Instruction in Tanzania Secondary Schools: Problems and Prospects. In Brock-Utne, Desai and Qorro (eds.): *LOITASA research in progress*. Dar es Salaam: KAD Associates.
- Wanjala, F.S. (2002). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiiri: Kwa Shule, Vyuvo na Ndaki*, Mwanza: Serengeti Educational Publishers.